
BIASHARA

PORI AKIBA LIPARAMBA

# Penye tembo wakimbizi, simba weupe na miti inayogeuka jiwe

- Maajabu ya maji yanayounda mchora wa ramani Afrika
- Ndege wa kilo 16, kumchinja kibali maalum serikalini



Mfano wa ramani ya Afrika iliyochorwa kwa maji juu ya mwamba, ndani ya Hifadhi ya Liparamba. **PICHA: GIDEON MWAKANOSYA**

**Na Gideon Mwakanosya,** MBINGA

KATIKA utaalamu na mfumo wa mbuga, pia hifadhi za wanyamapori, ni chache zilizobahatika kuwa na maingilio au mapitio ya wanyama ambayo yana jina mahsusi, ushoroba, kutoka nchi moja kwenda nyingine jirani.

Pori la wanyamapori Liparamba lililopo wilayani Nyasa mkoa wa Ruvuma, ni miongoni imo katika orodha ya mapori au mbuga za wanyama zilizobahatika na hilo.

Ofisa Utalii wa pori hilo, Maajabu Mbogo, anasema lilianzishwa mwaka 2000 na hadi sasa lina wanyamapori wakubwa na wadogo, wakiwamo tembo, simba, chui, viboko, mamba, tandala, pofu, palapala, kuro, nyati, pundamilia, fisi na mbweha.

Mbogo anaeleza kuwa, katika pori hilo kuna aina mbalimbali za ndege kama vile kanga, mbawala na fundichuma.

"Neno Liparamba ni la kabila la kimatengo ambao ni wenyeji wanaoishi wilaya ya Mbinga. Maana ya Liparamba, ni mbuzimawe," anasema Mbogo na kuendelea:

"Pori hili lina makundi makubwa ya tembo, ambao ni wakimbizi, kwa sababu huwa wanatoka Msumbiji na kuhamia Liparamba."

> **"Neno Liparamba ni la kabila la kimatengo ambao ni wenyeji wanaoishi wilaya ya Mbinga. Maana ya Liparamba, ni mbuzimawe.**

Anasema makundi makubwa ya tembo wanaotoka Msumbiji, huanza kuingia kwa wingi katika pori la Liparamba kuanzia mwezi Machi wanakoendesha maisha kwa wastani wa miezi minne na kisha Julai, tembo wanaanza safari ya kurudi Msumbiji.

Mbogo anasema, katika ya mwezi Septemba na Oktoba ya mwaka, mahali hapo panabakiwa na tembo wachache sana. Anaendelea na kufafanua:

"Inapotokea kule nchini Msumbiji majangili yamewashambulia tembo au kuwasumbua, tembo hao wanapoingia katika hifadhi ya Liparamba hawatoki. Wanaweza ndani ya pori la Liparamba kati ya miaka miwili hadi mitatu bila kutoka kurudi Msumbiji, kwa sababu Liparamba ni sehemu salama ya kuishi tembo."

Ofisa Utalii huyo anataja maajabu mengine yaliyopo Liparamba, kwamba kumeshawahi kuonekana simba mweupe na analitetea hilo kuwa si jambo geni au la ajabu mahali hapo.

Anavitaja vivutio vingine vilivyopo Liparamba, ni aina mbalimbali za nyoka kama vile jamii ya mamba na kobra, maporomoko ya maji ya Nakatuta katika Mto Ruvuma, ambayo ni kivutio cha asili cha utalii.

**MAAJABU&MTI JIWE**

Kwa mujibu wa Ofisa Utalii huyo, ni pori lenye vivutio vinavyofaa kufanya utalii wa kupanda kwenye mawe, ikizingatiwa yapo mengi makubwa na yanafaa kwa utalii wa aina hiyo.

Pia, anataja ndani ya pori hilo kuna utajiri wa miti, akitaja aina ya mtetereka, ambao ukikauka unabadilika kuwa jiwe na na inapatikana kwa wingi katika eneo la Nakatuta, kando ya Mto Ruvuma, kivutio kinachowateka watalii wengi wapenzi watafiti wa miti na mimea.

Mbogo anasema, katika eneo la Nakatuta, pia kuna miti mingine jamii ya kamba ambayo inapokatika, hutoa maji yanayonyweka, mithili ya maji kutoka vyanzo vingine na kukata kiu.

Ofisa Utalii huyo anasema, katika pori hilo kuna mito inayovutia, Mto Lumeme unaomwaga maji katika Mto Ruvuma na kuna mto usiokauka uitwao Lumeme na unaofaa kwa utalii wa kuogelea na kuvua samaki.

Analitaja eneo lingine linalofaa kwa utalii porini humo, ni makutano kati ya Mto Ruvuma na Mto Namakunguru, kwenye jiwe kubwa lenye urefu wa mita 70 kutoka chini ya Mto Ruvuma hadi juu, linalofaa kwa utalii wa kupanda.

Eneo la Mkuyu ndani ya Pori la Liparamba, kuna kivutio kinachowashangaza wengi na maji yanayotiririka kwenye Mto Mkuyu, yametengeneza mfano wa ramani ya Afrika juu ya mwamba.

"Maji yameweza kutengeneza mfano wa ramani ya Afrika juu ya mwamba. Ukichukua ramani ya Afrika na kuangalia ramani iliyotengezwa na maji, hakuna tofauti ni ramani kabisa ya Afrika, haya ni moja ya maajabu katika pori la Liparamba," anasema.

**HUDUMA YA MGENI**

Mhifadhi Msaidizi wa pori hilo, Paul Protas, anasema kila mgeni anapofika katika pori la Akiba Liparamba, anaweza kupata nafasi ya kutembelea Bwawa la Mkuyu ambako mtalii anapata nafasi kuogelea na kufanya utalii wa kuvua samaki na kumrudisha ndani ya maji.

Protasi anakitaja kivutio kingine ndani ya pori hilo, ni kuwapo wa ndege aina ya koribustard (Mbawala), ambaye nchini anatumika kama alama ya Taifa.

"Huyu ni ndege mkubwa ana uwezo wa kufikisha uzito kilo 16, ana urefu wa sentimeta 1330. Huyo ni ndege wa kitaifa, anachinjwa kwa kibali kinachoombwa kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania," anafafanua.

**OFISA UTALII MKOA**

Ofisa Maliasili wa Mkoa Ruvuma, Afrikanus Challe, anasema pori hilo lina kiwango cha juu cha hifadhi na inasimamiwa kisheria katika ulinzi, uendelezaji na matumizi ya busara ya mali hai, zikiwamo misitu, samaki na wanyamapori.

Utafiti umebaini kuwa pori Liparamba, ni eneo kipekee katika ukanda wa juu wa misitu ya miombo, ambalo lipo karibu na Ziwa Nyasa na uwapo wa msitu mpana wa asili na wenye mandhari ya kuvutia na eneo muhimu la kuhamia wanyamapori kati ya Tanzania na Msumbiji.

Anasema, serikali chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii, imelenga kutenga eneo hilo pawe kielelezo cha ukanda wa viumbehai katika mazingira yao ya asili, kwa kupunguza kasi ya mabadiliko makubwa yatokanayo na uharibifu wa kibinadamu, itokanao na sababu mbalimbali.

Ni jambo ambalo sasa Challe anasema, ni sehemu ya utafiti wa mazingira, elimu ya uchunguzi wa miti, wanyama na samaki.

Scanned with CamScanner